Tangazo la Serikali Na. 3 Limetolewa Tarehe 4/1/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

_____

AMRI

_____

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d))

AMRI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KAHAMA SHINYANGA("KASHWASA") (YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2018

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga("KASHWASA") (ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2018.

Tarehe ya kuanza

2. Amri hii itaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Januari 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za KASHWASA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo-

(a) ifikapo tarehe 30 Aprili 2019 au kabla, KASHWASA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) KASHWASA itatekeleza miradi kwa kutumia

fedha za ndani kama ilivyo katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(c) KASHWASA itawasilisha, kila baada ya miezi sita maendeleo ya hatua zilizochukuliwa katika kupunguza gharama za umeme kwa ajili ya uzalishaji wa majisafi;

(d) KASHWASA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

(e) KASHWASA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa KASHWASA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na KASHWASA katika siku zijazo.

Kutenguliwa kwa Amri

5. Amri hii inatengua matumizi ya Amri Na. 2015-005 ya tarehe 1 Septemba 2015 katika maeneo yanayohudumiwa na KASHWASA.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

BEI ZILIZOIDHINISHWA

Bei za Maji ya Jumla (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Bei za sasa	Bei Zilizopendekezwa			Bei Zilizoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	2018/19	2019/20	2020/21
Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira (WSSAs)	580	848	970	1,075	800	900	985
Muungano wa Jamii zinazosimamia Huduma za Majisafi (COWSOs)	435	636	730	810	600	675	740
Madini (WDL)	1,000	1,250	1,450	1,580	1240	1240	1240
Wastani wa Ulinganisho (WSSAs and COWSOs.	**569**	**832**	**952**	**1055**	**785**	**883**	**966**

JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA KWA KUTUMIA MAPATO YA NDANI YATOKANAYO NA BEI (SHILINGI KWA MILIONI)

Lengo	Shughuli itakayotekelezwa	2018/19	2019/20	2020/21
Ukarabati na Kubadilisha				
Dira zote zisizo fanya kazi iasavyo kubadilishwa ifikapo Juni 2021.	Kununua na kufunga dira za mtiririko wa umeme 24	142.80	28	88
Teknolojia iliyopitwa na wakati kubadilishwa ifikapo Desemba 2021.	Kununua na kufunga *speed drives* kwa ajili ya pampu za maji ghafi na pampu kwa ajili ya kusafisha mitambo.	37	15	70

Tangazo la Serikali Na. 3 (linaendelea)

Lengo	Shughuli itakayotekelezwa	2018/19	2019/20	2020/21
	Kuongezea vifaa kwenye *soft starters* zilizopo kwa ajili ya kuinua pampu za maji.	37	15	70
Nafasi ya kutosha kwa ofisi na makazi kupatikana ifikapo Desemba 2021.	Kukarabati nyumba za wafanyakazi Mwawile.	0	0	20
Mifumo ya utendaji na kuunganisha mifumo kufanya kazi yenyewe ifikapo Desemba 2021	Kuboresha mifumo ya kuandaa Ankara, uhasibu na malipo ya wafanyakazi.	0	0	70
Miradi Mipya				
Nafasi ya kutosha kwa ofisi na makazi kupatikana ifikapo Desemba 2021.	Kujenga ofisi ndogo Solwa.			50
Mifumo ya utendaji na kuunganisha mifumo kufanya kazi yenyewe ifikapo Desemba 2021.	Kufufua *Programmable Logic Controller (PLC).*	0	140	0
Usafiri wa kutosha kupatikana wakati wote.	Kununua magari mapya 8 (3 kwa mwaka wa pili na 5 kwa mwaka wa tatu) na pikipiki 16 (2 kwa mwaka wa kwanza na 14 kwa mwaka wa tatu).	5	320	515
Vitendea kazi kupatikana wakati wote.	Kununua vitendea kazi kama tarakilishi, printa na mashine ya kutoa nakala.	33.10	21.30	21.30
Kuendeleza na kudumisha mipango ya matengenezo ili kuboresha upatiakanaji wa huduma.	Kununua vitendea kazi vingine kama vile sanduku la vifaa.	54.78	20	20
	Kununua na kubadilisha *valves* zisizofanya kazi na viungio vingine kama vile *hydraulic control, butterfly na Needle valves*.	255.50	271.50	203.94
	Kufidia wakazi wanaopisha miradi ya maji.	0		50
	Kununua mfumo wa kuwekea madawa ya yanayoua wadudu (Chlorine) katika maji katika maeneo ya Old Shinyanga, Kishapu and Ngudu.	40	40	40

Tangazo la Serikali Na. 3 (linaendelea)

Lengo	Shughuli itakayotekelezwa	2018/19	2019/20	2020/21
Ulinzi katika vyanzo vya maji kuimarishwa muda wote.	Kuboresha kituo cha polisi katika vyanzo vya maji kwa kuongeza polisi na kujenga jengo jipya la polisi.			60
Ulinzi katika vyanzo vya maji kuimarishwa muda wote.	Kufanya tathmini ya ardhi kwa ajili ya usafirishaji wa bomba kuu na kupata hati za ardhi.	25	25	25
Mifumo ya utendaji na kuunganisha mifumo kufanya kazi yenyewe ifikapo Desemba 2021	Kuainisha mali zote za KASHWASA kama vile mifumo ya maji, dira na kuziweka kwenye mifumo ya GIS na SCADA kurahisisha usimamizi.	0	11.5	160
	Kuunganisha mfumo wa SCADA na mfumo wa kuandaa ankara.	0	0	15
Jumla ya Gharama Zote		**630**	**907**	**1,428**

Dodoma,
....., 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu

Tangazo la Serikali Na. 3 (linaendelea)

_____